

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Zanzibar
20 Agosti, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema Tamasha la Kizimkazi limeendelea kujipambanua kuwa la kimaendeleo kwa kuchochea utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye manufaa makubwa kwa wananchi.

Rais Dkt. Samia amesema hayo wakati akifungua Skuli ya Maandalizi Tasani iliyoko Makunduchi na kusisitiza kuwa njia nzuri ya kuwalinda watoto ni kuhakikisha kuwa wanapata fursa ya kusoma.

Aidha, Rais Dkt. Samia amewataka walezi wa kituo hicho kuwalea watoto kimaadili na kiakili kwa kuzingatia misingi ya Malezi ya Awali ya Mtoto (ECD).

Rais Dkt. Samia amesema Serikali ina dhamira ya kuhakikisha kwamba watoto wote nchini wanapata malezi bora ikiwemo maandalizi mazuri yatakayowapa msingi mzuri wa mafanikio shuleni na maishani.

Katika hafla ya kuhitimisha mafunzo na kugawa vyeti kwa washiriki wa mafunzo ya ujasiriamali, Rais Dkt. Samia amewataka vijana kuchangamkia fursa za kupata mafunzo na ujuzi mbalimbali ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Rais Dkt. Samia pia amewataka wahitimu waliopata mafunzo kufanya shughuli za kiuchumi za kilimo, utalii na uvuvi huku wakitunza mazingira, mila na desturi ambazo ndizo zinawavutia watalii kuja Zanzibar.

Kupitia Tamasha la Kizimkazi jumla ya vijana 607 wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali pamoja na kilimo, uvuvi mifugo, utalii na sanaa ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Tamasha la Kizimkazi la mwaka 2024.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Sharifa B. Nyanga'.

Sharifa B. Nyanga
Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

